

## SUNNAH ZA SWAUMU.

1. Kula daku Mtume (saw) anasema:

(Kulen i daku kwani kwenye kula daku kuna Baraka) (ameipokea Bukhar na Muslim:1923, 1095).

Na katika sunnah ya kula daku ni kuchelesha daku mpaka mwisho wa usiku kwa Hadith ya Mtume (saw) inayosema:

(Hautaacha kuwa Ummat wangu kwenye kheri watakapofanya haraka kufungua na kuchelewesha kula daku) (Imepokelewa Sahih Ja'ami:2835).

2. Kufanya haraka kufungua pindi itakapo hakikiya kuwa jua limezama, na sunnah ya kufungua ni kufungua na tende ukikosa tende, basi fungua kwa kutumia maji na ukikosa maji utafungua na chochote kilichokuwa ni wepesi kwako.

3. Kuomba wakati wa kufunga na hasa hasa wakati wa kufunga kwa hadithi ya Mtume (saw) anasema:

(Mtume swalallahu Alayhi wa Salaam anasema: Dua za watu watatu ni zenyeku kubaliwa, Dua ya mwenye kufunga, Dua ya mwenye kudhulumiwa, na Dua ya msafiri) (Ameipokea Albaihaqiy).

Na yale yanayotakikana kwa mfungaji ni kisimamo katika mwezi wa Ramadhan kwa Hadithi ya Mtume (saw) aliposema:

(Mwenye kusimama mwezi wa Ramadhan hali ya kuwa ana Imaan na kutarajia malipo kutoka kwa Allah atasamehewa madhambi yake yaliyo tangulia) (Ameipokea Bukhar na Muslim:2009, 759).

Inatakikana kwa muislamu kukamilisha swala ya tarawehe pamoja na Imam kwa kauli yake Mtume (saw) aliposema:

(Mwenye kusimama pamoja na Imam wake kisimamo cha Ramadhan mpaka akamaliza ataandikiwa amesimama usiku) (Imepokelewa na Asw-habu sunani).

Na mionganoni mwa mambo ambayo yanatakikana mwezi wa Ramadhan ni kutoa swadaka kwa wingi sana.

Kama vile inavyotakiwa kujitahidi kusoma Quran kwa wingi kwenye mwezi wa Ramadhan na mwezi wa Ramadhan ni mwezi wa Quran, kwani mwenye kuisoma Quran kila herufi moja anapata thawabu kumi na jema moja ni thawabu kumi na mfano wake.

## SWALA YA TARAWEHE.

Tarawehe ni kisimamo cha usiku mwezi wa Ramadhan kusimama jama'a, wakati wake ni baada ya swala ya Ishai mpaka kuchomoza kwa alfajir, kwa hakika Mtume (saw) alitilia mkazo katika kusimama mwezi wa Ramadhan na ni sunnah kuswali rakaa kumi na moja na kutoa salamu kila baada ya rakaa mbili.

Atakapozidisha zaidi ya hizo rakaa kumi na moja hakuna tatizo, na katika sunnah za swala ya tarawehe kutokufanya haraka na kufanya kisomo kirefu kisichowapa tabu wenyewe kuswali.

Hakuna tatizo ikiwa watahudhuria kwenye swala ya tarawehe wanawake ikiwa hakuna fitna, kwa sharti la kutoka kwa heshima sio kudhihirisha mapambo yao wala kujipaka manukato.